

يجاب من أنكر عذاب القبر مجحجة أنه لو كشف القبر لوجد أنه لم يغير بعدة أجوبة منها: أولاً: أن عذاب القبر ثابت بالشرع، قال الله تعالى في آل فرعون: (الَّذِي أَنْهَا عَذَابُنَا عَلَيْهَا غَلَوْا وَغَيْرَهُمْ تَقْوَمُ السَّاعَةُ إِذَا خَلُوا آلَ فِرْعَوْنَ أَشَدُ الْعَذَابِ) (غافر: 46) قوله ﷺ: ((فَلَوْلَا أَنْ تَدَافَنَا لَدَعْوَتُ اللَّهَ أَنْ يَسْعَكُمْ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ الَّذِي أَسْعَى مُثْقَلَ بُوْجَهِ قَالَ: تَعُوذُوا بِاللَّهِ مِنْ عَذَابِ النَّارِ, قَالُوا نَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ عَذَابِ النَّارِ قَالَ: تَعُوذُوا بِاللَّهِ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ)). وقول النبي ﷺ في المؤمن ((يفسح له في قبره مد بصره))، إلى غير ذلك من النصوص فلا يجوز معارضته هذه النصوص بهم من القول، بل الواجب التصديق والإذعان. ثانياً: أن عذاب القبر على الروح في الأصل، وليس أمراً محسوساً على البدن، فلو كان أمراً محسوساً على البدن لم يكن من الإيمان بالغيب، ولم يكن للإيمان به فائدة، لكنه من أمور الغيب، وأحوال البرزخ لا تقام بأحوال الدنيا. ثالثاً: أن العذاب والتعيم وسعة القبر وضيقه، إنما يدركه الميت دون غيره، والإنسان قد يرى في المنام وهو نائم على فراشه أنه قائم وذاهب وراح، وضارب ومضروب، ويرى أنه في مكان ضيق موحش، أو في مكان واسع كييج، والذي حوله لا يرى ذلك ولا يشعر به. والواجب على الإنسان في مثل هذه الأمور أن يقول سمعنا وأطعنا، وآمنا وصدقنا.

**'Yule ambaye anapinga uwepo wa adhabu za kaburini kwa hoja ya kwamba ikiwa kaburi litafukuliwa atakutwa maiti hajabadilika (kwa sababu ya adhabu yoyote), atajibowi mtu huyo kwa majibu mbalimbali miongoni mwayo ni haya:**

**Kwanza:** Adhabu ya kaburini uwepo wake umethibitika kisheria, amesema Allah Mtukufu kuhusu wafuasi wa Firauni ; (( Watadhihirishiwa moto ndani ya makaburi yao asubuhi na jioni, na siku ya Qiyama itasemwa, waingizeni watu wa Firauni katika adhabu nzito mno)) Ghaafir 46; Na kauli ya Mtume swallallaahu alaihi wasallam (( Na laiti msingezikwa (baada ya kufa kwenu) ningemuomba Allah akusikilizisheni adhabu za kaburini ambazo mimi nazisikia, kisha akageuza uso wake akasema: 'Ombeni kinga kwa Allah dhidi ya adhabu ya moto' ; wakasema Maswahaba; ' Tunajikinga kwa Allah dhidi ya adhabu ya moto'; kisha akasema tena; 'Ombeni kinga kwa Allah dhidi ya adhabu ya moto' ; wakasema Maswahaba; ' Tunajikinga kwa Allah dhidi ya adhabu ya moto' )). Na kauli yake aliposema kuhusu muumini (atayesalimishwa na adhabu za kaburini), (( litapanuliwa kaburi lake umbali wa upeo wa macho yake)); na nyinginezo katika dalili za kisheria ambazo haifai kuzipinga kwa kutumia dhana , bali ni wajibu kuzisadikisha na kunyenyea.

**Pili ; Asili ya adhabu za kaburini ipo juu ya roho (ya maiti) na sio jambo lenye kuonekana katika mwili wa maiti (tulyiemzika), lau kama lingekuwa ni jambo la kuonekana katika mwili wa maiti basi adhabu ya kaburini isinge kuwa miongoni mwa imani ya ghaibu (yaliyofichikana); na isinge kuwepo faida yoyote ya kuamini ghaibu (yaliyofichikana). Bali adhabu ya kaburi ni miongoni mwa mambo yaliyofichikana, na hali za (matukio ya) kaburini haziwezi kupimwa kwa hali (za matukio) ya kidunia.**

**Tatu :** Hakika adhabu za kaburini na neema zake na upana wa kaburi na ufinyu wake ni mambo ambayo anayaafahamu maiti mwenyewe, si mwingine asiyekuwa yeye. (Mfano) mtu aliylala usingizini akiwa kitandani kwake anaweza kuota ndotoni kuwa amesimama au ameondoka na akarejea, au amepiga au amepigwa , au akaota yupo katika eneo finyu mno linalobana lenye kutisha; hali ya kuwa mtu mwingine aliyepembezoni mwake haoni yote hayo wala hapati hisia yoyote kuhusu hayo (anayaona mwenzake ndotoni).

**Na wajibu ulio juu ya kila mtu katika mfano wa mambo haya ya ghaibu (yaliyofichikana) ni aseme tumesikia na tumetii na tumeaminu na tumesadikisha (tumekubali).'**

**Mwisho;**

وصلى الله على محمد وعلى آله وصحبه وسلم